

Sauti za ndege asubuhi!



LIDA Portugal ✎
Vilius Aistis Vilimas ✉
Jacob Haule 📄
5 🗳️
Kiswahili! 🗣️ MS




LIDA Stories

lidastories.net

Sauti za ndege asubuhi!

LIDA Portugal ✎
Vilius Aistis Vilimas ✉
Jacob Haule 📄




This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Yulia, mume wake, na binti yao mdogo walikuwa wakiishi katika kijiji kidogo chenye ukimya nchini Ukraini. Yulia alipenda kuamshwa na sauti za ndege kila siku. Hakuwahi kufikiria kuwa angekuja kuishi mbali na nyumbani au kutoamshwa na sauti za ndege asubuhi.


Mume wake, kwa upande mwingine,
alikuwa akilalamika sana kuwa hana pesa
ya kutosha na akaanza kunywa pombe
vibaya. Wakaamua kujaribu bahati yao
Ureno. Labda hukoo wangepweza kupata
pesa zaidi za kujenga nyumba na
wakaiandalia familia yao maisha mazuri ya
baadaye.






Yulia alizoea vizuri makazi yake mapya na alianza kufanya kazi kama mfanyakazi wa usafi. Wateja wake walimpenda sana kwa jinsi alivyofanya kazi kwa bidii na heshima yake. Kwa upande mwingine, mume wake alijihisi anatengwa zaidi na zaidi. Kwa sababu ya tatizo lake la ulevi, waajiri hawakuwa na imani naye na hawakutaka kumpa kazi.

Siku moja, alianza kumgombeza Yulia. Kisha, akaanza kumsukuma. Kelele na vipigo vikafikia hatua mbaya, hasa akiwa amelewa. Yulia alilogopa na aliingwa na wasiwasi kuhusu binti yake lakini hakuwa na la kutanya.




Yulia akaenda katika makazi ya wanawake ambapo alijihisi salama kuliko alivyokuwa kwa muda mrefu. Hakuwahi kujisikia hivyo tangu aliipoamshwa na sauti za ndege asubuhi.





Hatimaye, wakati Yulia alilazimika kwenda kwenye chumba cha dharura akiwa amevunjika mkono, walimwambia kuwa unyanyasaji wa majumbani ni tatizo kubwa nchini Ureno. Pia walisema kwamba ilikuwa ni kosa na anapaswa kuripoti polisi.



Yulia alikuwa amechoka na hakutaka binti yake mdogo kukua katika mazingira ambayo anashuhudia unyanyasaji kila siku. Yulia alitambua kuwa viashiria vya unyanyasaji vilishakuwepo tangu kitambo hata kama vilikuwa vya namna tofauti.